# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA ISHIRINI NA NANE

**20 MEI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA ISHIRINI NA NANE - TAREHE 20 MEI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA KILIMO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga

Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## III. MASWALI:

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**351 MHESHIMIWA DKT. PIUS STEPHEN CHAYA (MANYONI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kurasimisha Viongozi wa Nyumba Kumi (Mabalozi) kama sehemu ya kuimarisha usalama wa raia.

**352 MHESHIMIWA ZUENA ATHUMANI BUSHIRI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Uchira – Kisomachi katika Jimbo la Vunjo.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**353 MHESHIMIWA MOHAMMED JUMAH SOUD (DONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, kwa nini NEMC haianzishi utaratibu wa kuishirikisha ZEMA ili kuongeza ufanisi wa uibuaji na usimamizi wa Miradi ya Mazingira Zanzibar.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**354 MHESHIMIWA NOAH LEMBURIS SAPUTU (ARUMERU MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itakarabati Mnada wa Olokii uliopo Kata ya Bwawani - Arumeru Magharibi.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**355 MHESHIMIWA FATMA HASSAN TOUFIQ (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, ipi kauli ya Serikali kuhusu Wasichana waliopata mimba kutokana na kubakwa na wanaopewa mimba na baba zao au ndugu wa karibu.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**356 MHESHIMIWA NAJMA MURTAZA GIGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta Muswada wa Sheria ya kuwalinda Watoto wa Kike wanaofanyiwa vitendo vya usagaji nchini.

**WIZARA YA AFYA:**

**357 MHESHIMIWA STELLA IKUPA ALEX (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, upi mkakati wa Serikali wa kutoa dawa bure kwa Wagonjwa wa Akili.

**358 MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati miundombinu ya Hospitali ya Kitete - Tabora yenye miaka zaidi ya 100.

**WIZARA YA MAJI:**

**359 MHESHIMIWA ESTHER EDWIN MALLEKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha miundombinu ya Maji Safi na Salama kwa Wakazi wa Kilimanjaro.

**360 MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE (NDANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Miradi ya Maji ya Nambawala, Chiwata, Mbemba, Ndanda na Nanganga itakamilika.

**WIZARA YA MADINI:**

**361 MHESHIMIWA YAHYA ALLY MHATA (NANYUMBU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA
UHURU NA UMOJA

Je, fedha kiasi gani zimepatikana kutokana na Madini katika Wilaya ya Nanyumbu kuanzia Mwaka 2020 mpaka 2023.

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**362 MHESHIMIWA LUCY JOHN SABU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Sekta ya Sanaa na Michezo inawanufaisha Vijana kwa kuweka mifumo rasmi.

**WIZARA YA UJENZI:**

**363 MHESHIMIWA DKT. CHRISTINA CHRISTOPHER MNZAVA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Kagongwa - Isagahe - Bukene hadi Nzega.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **20 MEI, 2025** | **KATIBU WA BUNGE** |